# UFUNDISHAJI WA KUSOMA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NA VYUO

*F.L. Mbunda*

Kitabu cha *Kufundisha Kusoma*[1] kimeelezea taratibu na matatizo ya *Kusoma* hususa katika shule za msingi. Utangulizi wa kitabu hiki unatoa maelezo kuhusu umuhimu wa kujua kusoma, sura ya kwanza inatoa maelezo zaidi juu ya haja ya kujua kusoma, pamoja na mazingira yanayoambatana na ustadi katika kusoma.

Kwa kuwa kusoma ni shughuli isiyo na kikomo itakuwa bora iwapo mawaidha yatatolewa ambayo yatagusia kanuni na ufundishaji wake katika viwango zaidi ya shule za msingi. Shabaha ya makala haya ni kuwasaidia walimu na wakufunzi katika kulimudu somo la *Kusoma* katika shule na vyuo. Vipengele ambavyo vimegusiwa katika makala haya ni:-

(a) *Kusoma* ni nini? Hii itatusaidia kulielewa somo lenyewe kabla ya kulimudu.

(b) Stadi katika *Kusoma*. Kila somo lina stadi zake ambazo kila mwanafunzi itambidi azizingatie.

(c) Aina za *Kusoma* ambazo zinategemewa kuwa zitakidhi haja na matakwa ya kila mwanafunzi.

(d) Shabaha katika *Kusoma*. Kila somo lina malengo yake, bila hayo tutajikuta hatuelewi tuendako.

(e) Njia za Ufundishaji zitatusaidia katika kulimudu somo la *Kusoma* ndani na nje ya darasa.

Kila kipengele sasa kitafafanuliwa kwa kifupi kama itakavyofuata hapa chini. Mawaidha zaidi kuhusu suala zima la kusoma yataweza kupatikana kutoka kitabu cha *Kusoma kwa Ufahamu*[2].

## 1. *KUSOMA NI NINI?*

*Mara nyingi Kusoma* kunachukuliwa kama uwezo wa kutambua maneno na kufahamu yaliyomo. Na mara chache tunafikiria matokeo kwa msomaji na jinsi anavyoweza kuyayeyusha yale aliyoyasoma. Hali kadhalika msomaji haelekezwi kuona umuhimu wa yale aliyosoma, akayahakiki na kuweza kugundua uwiano na mambo yaliyomsibu katika maisha. Hayo yote ni matokeo ya stadi katika *Kusoma*. Kazi hii ya *Kusoma* ni mchanganyiko wa shughuli nyingi ambazo zinahusisha kuona na kufikiri kwa upande wa msomaji.

Wataalamu wengi siku hizi wamejaribu kutoa maana mbali mbali za *Kusoma* wakifikiria hasa kile kinachotendeka wakati huo pamoja na matokeo yake.

---

1. F.L. Mbunda: Oxford University Press (1974)
2. F.L. Mbunda: Shungwaya Publishers Ltd., (Mswada)

Wataalamu fulani wanaona *Kusoma* ni njia ya kutambua na kubaini maandishi kwa upesi na kwa usahihi, kufikia kiwango cha kutosha cha kuelewa maana iliyokusudiwa na mwandishi, na kuitumia ile maana iliyofikiwa.

Wengine wanafikiri *Kusoma* ni kufasiri na kuainisha mawazo yaliyomo katika maandishi. Wao wanaona kuwa *Kusoma* ni utaratibu wa mawasiliano na msomaji. Katika utaratibu huo panatokea kuwa na *chanzo, mpelekaji, kiwakilisho, mpokeaji* na *kikomo*. *Chanzo* na *mpelekaji* ndio wanaounda *fumbo* ambalo linajificha katika maandishi [*kiwakilisho*] na *mpokeaji* na *kikomo* ndio wanaofumbua hilo *fumbo* kwa kuyatafsiri mawazo yaliyomo.[3]

Kutokana na maana hizo za *Kusoma* tunaweza kuzichambua shughuli nne ambazo tunazitegemea kuwapo kila tunaposoma au kufundisha *Kusoma*:-

(1) *Utambuzi wa Maneno*:- Hii ni shughuli ya kulipa neno maana yake mara moja. Maneno yaliyomo yanapatiwa maana yake kwa kuhusisha na maana ambayo mwandishi ameikusudia.

(2) *Ufahamu wa Mawazo*:- Sehemu hii inashughulika na kuona maana ya maneno kama yalivyotumiwa na kutambua mawazo yaliyomo. Katika hatua hii msomaji anahusisha maandishi na mazingira yake pamoja na maisha kwa ujumla ili kupata mawazo, maono na maana iliyokusudiwa na mwandishi.

(3) *Tafsiri ya Mawazo*:- Hapa msomaji anaelekea na kuchambua mawazo aliyosoma, anayapima, na kuyapokea au kuyakataa kufuatana na jinsi yalivyomwingia.

(4) *Uzingatiaji*:-Msomaji anayashikilia yale yenye maana na kuyafanya sehemu ya maisha yake. Yale ya maana yaweza kuwa mawazo (maarifa) au lugha iliyomo ambayo yanachanganywa na ya msomaji, na hivi kukuza au kupanua maisha kwa ujumla.

Shughuli zote nne zinategemeana na kuhusiana. Mathalani msomaji hawezi kuzingatia yenye maana kama hakutambua maneno na lugha iliyomo, au kufahamu na kuchambua mawazo yaliyomo. Baada ya shughuli zote kutimizwa sawa sawa ndipo tunaweza kusema kuwa 'fulani amesoma.'

## 11. STADI KATIKA KUSOMA

Kutokana na maelezo kuhusu kile kinachotokea wakati wa kusoma inatubidi tuangalie mategemeo yetu katika *Kusoma,* yaani, msomaji atatakiwa kuwa na stadi gani katika shughuli zote nne. Stadi hizo ndizo zitakazoamua kiwango cha mwanafunzi katika ufundi wa kusoma. Stadi hizo ni uwezo wa mwanafunzi katika kutambua maumbo na maana ya maneno kwa haraka iwezekanavyo; ufahamu wa habari kutokana na ugunduzi, uchaguzi, upangaji na uzingatiaji wa maarifa, utambuzi wa miundo ya maneno katika kusaidia kupata maana, na wepesi katika kusoma kukizingatia matamshi, lafudhi na vituo.

*Kusoma* basi ni mkusanyiko wa shughuli nyingi. Kujifunza *Kusoma* sio kazi nyepesi kama inavyodhaniwa. Ni kazi inayoendelea hata katika kiwango cha sekondari, vyuo vikuu, au katika utu uzima au uzeeni. Kila tusomapo tunategemea kupata mambo mapya, kurekebisha misimamo yetu, na kutoa maono kutokana na hali mpya iliyopatikana.

3. **Mawazo kama yanavyotolewa na R. Karlin katika 'Teaching Reading in the High School': Bobbs—Merrill (1964).**

## 111. AINA ZA KUSOMA

*Kusoma* kukichukuliwa kama shughuli isiyo na kikomo, hatuwezi tukasema kwamba kufundishwa kwake kunaishia katika shule za msingi. Kama ni vile, lazima pawepo na utaratibu maalum wa *Kusoma* kama somo hilo litatakiwa kufana katika hali zote. Katika kutekeleza lengo hilo *Kusoma* shuleni na vyuoni kunagawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

1. *Kusoma kwa ajili ya kukuza maendeleo*: Sehemu hii inahusiana na ratiba maalum ambayo inafundishwa kwa wote hata kama maendeleo yao ni tofauti. Shabaha yake ni kumwezesha mwanafunzi apate misingi katika *Kusoma* na kujiendeleza kufuatana na uwezo wake. Ni utaratibu unaofuatana na madhumuni ya elimu kwa ujumla, na kumkuza mwanafunzi katika hali zote. Ni utaratibu ambao una viwango maalum kwa kufuatana na madarasa, uwezo na mahitaji ya wanafunzi. Ni mpango ambao unaendelea kila siku na katika kila somo.

2. *Kusoma kwa ajili ya kurekebisha makosa:* Mpango huu unatokea kila shida iwapo. Mwalimu darasani anatumia njia na vifaa mbali mbali katika kurekebisha kosa fulani lililojitokeza kwa mwanafunzi, kikundi cha wanafunzi au darasa zima.

3. *Kusoma kwa ajili ya kuzuia makosa:* Mwalimu anaweza kutabiri uwezekano wa makosa fulani fulani baina ya wanafunzi wake. Hivyo yambidi kutumia njia fulani zozote zile ili mradi makosa ya aina hiyö yasitokee. Kwa upande mwingine, mwalimu anaporekebisha makosa kwa kweli anazuia makosa.

Kusoma kwa aina zote tatu ni muhimu sana katika kila hali ya ufundishaji *Kusoma.* Faida yake ni kwamba kila mwanafunzi anapewa kile anachohitaji kutegemeana na uwezo, matakwa na haja zake. Lakini hata hivyo *Kusoma* kwa ajili ya kukuza maendeleo ni msingi wa shughuli zote za *Kusoma. Kusoma* huko kunamfanya mwanafunzi ajipatie maarifa mapya kila wakati na papo hapo kuendeleza stadi zake katika *Kusoma.* Stadi hizo zitamsaidia mwanafunzi katika kukabili mambo mengi yanayomzunguka na yatakayomzunguka.

Tunapoangalia *Kusoma* kwa ajili ya kukuza maendeleo katika shule za sekondari na vyuo tunapambana na pande mbili za *Kusoma* huko. Kuna kule *Kusoma* ambako msingi wake ni kujiendeleza katika uwezo na mazoea katika *Kusoma.* Pia, kuna kusoma kwa ajili ya kujifundisha; shabaha yake ikiwa kujenga hamu na ari katika *Kusoma.* Moyo ukisha jengeka tunafikiria kwamba patakuwepo na misingi ya kudumu katika *Kusoma.*

*Kusoma* katika sehemu zote mbili kutawezekana tu iwapo kuna shabaha na utaratibu maalum. Baada ya kuona lengo ni nini ndipo tunaweza kuchagua mbinu, vifaa na njia ambazo zitatosheleza hizo shabaha. Hii itamwezesha mwanafunzi kufuata na kujifunza vema kwa sababu mambo anayopata yanalingana na mahitaji yake ambayo yameelekezwa katika shabaha zilizotolewa.

## IV. SHABAHA KATIKA KUSOMA

Katika *Kusoma* tunaweza kufikiria kwa ujumla shabaha zifuatazo:-

1. Kukuza na kuendeleza msamiati, yaani lugha kwa ujumla.
2. Kupanua mawazo kutokana na kila kisomwacho.
3. Kukuza uwezo wa ufahamu na uchambuzi wa maandishi ili kupata maana zilizomo.

4 . Kukuza stadi za upekuzi wa maandishi ili kuona uzuri au uhafifu wake.
5 . Kukuza uwezo wa kupanga mawazo kutokana na maandishi na uwezo wa kuyatumia katika mazingira mapya.
6 . Kukuza mwendo wa kusoma kwa ajili ya madhumuni mbalimbali ikiwa ni kwa kusoma kimakini au kupitia juu juu tu.
7 . Kuweza kugundua, kuchagua na kupanga mawazo yatokanayo na *Kusoma.*
8 . Kuendeleza hamu ya kupenda *Kusoma* na kuthamini yaliyomo.
9 . Kutoa mwongozo na mazoezi katika aina mbalimbali za kusoma, kwa mfano kusoma katika masomo mengine kama historia, sayansi, hesabu n.k.
10 . Kusaidia maendeleo (katika kukua) ya mwanafunzi binafsi.

Hizo ni shabaha za jumla, lakini kila somo la *Kusoma* litakuwa na shabaha zake kwa ajili ya stadi maalum kama mwalimu atakavyopanga. Shabaha hizo pamoja na shughuli zake katika *Kusoma* ndizo zinazoeleza maana na umuhimu wa *Kusoma.* Mwalimu basi itampasa ahusishe shughuli katika kusoma na shabaha zake. Shabaha ndizo zitakazoamua jambo na njia za kufundisha *Kusoma.*

## V. NJIA ZA UFUNDISHAJI

Muhtasari wa Kiswahili kwa shule za sekondari unagusia somo la kusoma katika *Kusoma* na *Ufahamu* na katika *Muhtasari* [*Ufupisho*]. Hali hiyo hiyo imo katika muhtasari ya Vyuo vya Elimu ya Taifa. Tusisahau pia kuwa stadi ya kusoma itahitajika sana katika somo la Fasihi. Kufanikiwa kwa Fasihi kutategemeana sana uzingatiaji wa somo la *Kusoma.*

Jambo la muhimu kwa mwalimu au mkufunzi kwanza ni kuelewa Taifa lina madhumuni gani kwa upande wa elimu, na hali kadhalika shabaha katika somo la *Kusoma.* Pili, itambidi mwalimu achague na kuandaa vifaa vyote vitakavyotakikana kufuatana na viwango vya mwanafunzi, na pia aina ya kusoma.

Karibu muhtasari yote imependekeza vitabu na vifaa vingine vya kujisomea. Lakini hii haina maana kwamba mwalimu au mkufunzi asitafute vifaa vingine licha ya vile vilivyopendekezwa katika muhtasari, hasa inapohusu aina mbalimbali za kusoma. Mathalan katika kusoma kwa ajili ya kukuza maendeleo ya wanafunzi, kurekebisha au kuzuia makosa, na katika kusoma kwa sauti na kwa kujifurahisha, mwalimu au mkufunzi awe huru kutafuta vitabu au makala yoyote yale, ila tu asiende nje na malengo ya Taifa, na ahakikishe kuwa vifaa hivyo vinalingana na uwezo, haja na matakwa ya wanafunzi.

Kazi ya tatu ni kuandaa somo lenyewe. Mkufunzi ahakikishe kwanza *kusudi la somo* lake (tazama sehemu IV). Halafu ahakikishe kuwa ana zana zitakazomsaidia kulingana na kusudi la somo. Zana hizo zaweza kuwa picha, chati au vitu halisi.

Ikibidi kutembelea mahali ambapo habari yake itasomwa basi yambidi mwalimu au mkufunzi aandae hivyo. Mwisho aonyeshe hatua kwa hatua jinsi atakavyoendesha somo darasani akizingatia shughuli za wanafunzi na zake mwenyewe tangu mwanzo hadi mwisho wa somo.

Somo lolote lile halina budi kupima au kutathmini maendeleo na viwango ambavyo wanafunzi wamefikia. Hii yote itategemeana na kusudi la somo la siku hiyo. Katika somo la *Kusoma* tunapima kama kusudi la somo limefikia kiwango

chake, na hali kadhalika, iwapo stadi zake zimezingatiwa vya kutosha. Umuhimu wa yote tunapima ufahamu wa yaliyosomwa katika viwango vyake mbalimbali. Viwango hivi ni vya:-

1. *Kumbukumbu* — kiasi gani wanafunzi wanakumbuka habari na mambo muhimu waliyoyasoma.

2. *Ufafanuzi* — kiasi ambacho wanafunzi wanaweza kutoa maana ya taarifa au msamiati kutoka kifungu walichokisoma.

3. *Kuhusisha* — jinsi wanafunzi wanavyoweza kuonyesha uwiano baina ya maarifa au lugha iliyomo.

4. *Utatuzi* — namna wanavyoweza kutatua vipengele mbalimbali katika habari, k.m. kuonyesha sababu za matukio fulani fulani.

5. *Uchanganuo* — kiasi ambacho wanafunzi wanaweza kudondoa kipengele kimoja kimoja kutoka jumla ya vipengele vyote.

6. *Uchangamano* — jinsi wanafunzi wawezavyo kukusanya vipengele mbalimbali ili kufanya kipengele kimoja, k.m. katika ufupisho au kutafuta kichwa cha habari.

7. *Uhakiki* — kiasi ambacho wataweza kupima ukweli au udhahiri wa mambo wakitoa maoni au msimamo wao kutokana na habari waliyosoma.

Tathmini katika kusoma itategemea sana aina ya *Kusoma.* Kwa mfano katika *kusoma kwa sauti* mambo yanayoweza kupimwa ni *wepesi wa kusoma, matamshi* na *lafudhi. Usikivu* wa yaliyosomwa ni muhimu kupimwa pia. Hii itahakikisha kwamba darasa zima walikuwa wakifuata au sivyo. Katika vyuo aina ya mazoezi yaweza pia kuwa ya kutunga maswali juu ya yale yaliyosomwa. Hili ni zoezi zuri katika kuwaandaa walimu wa baadaye.

Walimu na wakufunzi wataangalia pia kuwa hatua za somo zitalingana na aina ya *Kusoma.* Hatua zilizopendekezwa hapo juu ni kwa ajili ya kusoma darasani katika kukuza maendeleo ya wanafunzi. Iwapo kusoma ni nje ya darasa kwa ajili ya kujipatia maarifa au kujifurahisha, walimu na wakufunzi wawaongoze wanafunzi wao kufuata mazoea maalum. Kwa mfano katika kusoma ili kupata maarifa fulani au kwa ajili ya kazi maalum itafaa kufuata utaratibu ufuatao:-

1. Kuwa na lengo maalum.
2. Kusoma juu juu ili kupata mambo muhimu.
3. Kusoma kwa makini ili kutafuta jambo maalum.
4. Kujibu au kutatua jambo maalum.
5. Kusoma tena ili kulinganisha jibu na habari iliyosomwa.

Utaratibu kama huo utawafaa zaidi wanachuo vyuoni ambao wanajiandaa kuwa walimu.

Kusoma kwa kujifurahisha au kwa ziada kusimalizike hivi hivi tu. Itafaa wakati fulani fulani wanafunzi wazoezwe kuandika maono na uhakiki wa vitabu wasomavyo. Kwa njia hii walimu na wakufunzi watahakikisha maendeleo ya wanafunzi wao katika viwango na hali mbalimbali.

Misingi iliyotolewa katika makala haya ikizingatiwa haitasaidia kukuza stadi za kusoma tu, bali, itasaidia pia katika kukuza moyo wa kupenda kusoma, kujifunza katika masomo mbalimbali, na katika kufanikisha somo la Fasihi. Misingi hiyo ikiendelezwa, *Kusoma* hakutakuwa shughuli ya darasani tu, bali kutakuwa sehemu muhimu katika maisha yote ya wanafunzi kwani wanafunzi watajenga mazoea ambayo yanalingana na haja na matakwa yao.